

Sasa tuko na chanjo za kutukinga na COVID-19

HAPA CHINI KUNA YALE UNAHITAJI KUJUA



Chanjo zote ni salama na zinatoa kinga.

Chanjo bora ni ile ambayo unaweza kupata. Chanjo zote ambazo zimeidhinishwa nchini Marekani ni salama na zinatoa kinga ili kuzuia ugonjwa mkali na kifo. Kamati ya Chakula na Dawa ya Marekani (FDA) iliidhinisha chanjo hizo kwa matumizi ya dharura, na madaktari na wataalamu wa kibinafsi walithibitisha kuwa chanjo hizo zinafikia viwango vya juu vya usalama.

Chanjo hizo zinatolewa bila malipo.

Serikali ya shirikisho italipia gharama ya chanjo yako. Watoa huduma wanaweza kukutoza ada ya kukupea chanjo, lakini bima ya afya itaweza kuigharamia.

Huenda ukahitaji dozi mbili.

Kulingana na chanjo ambayo utapokea, huenda ukapokea dozi moja au mbili, na dozi ya pili utapokea katika muda wa wiki tatu hadi nne baada ya kupokea ya kwanza.

Unaweza kuhisi athari mbaya.

HUWEZI kuambukizwa COVID-19 kutoka kwa chanjo. Lakini kama chanjo zingine za kawaida, unaweza kupata mkono wenye kidonda, homa ya joto, maumivu ya kichwa au kuhisi uchovu baada ya kupata chanjo. Hizi ni ishara kwamba chanjo inafanya kazi.

Watu walio katika hatari kubwa zaidi hupata chanjo kwanza.

Dozi za kwanza zinaenda kwa wafanyakazi walio katika hatari kubwa ya kuambukizwa katika mipangilio ya huduma za afya. Kila mtu ataweza kupata chanjo wakati tuna kipimo cha kutosha. Nenda kwenye www.mass.gov/covid-19-vaccine ili kujua ni lini unaweza kupewa chanjo.

Watu wengine hawapaswi kupata chanjo.

Unaweza kupata chanjo hata kama umekuwa na COVID-19. Watoto walio na umri wa miaka chini ya 16 hawapaswi kupata chanjo. Unapaswa kumwambia mtu anayekupatia chanjo ikiwa una homa, una historia ya athari kali ya mizio, una shida ya kutokwa na damu au kama unatumia dawa za kuzuia damu kuganda, una shida za kinga ya mwili, au wewe ni mjamzito.

Kaa salama baada ya kupata chanjo.

Baada ya kupata chanjo, mnaweza kukutana mkiwa vikundi vidogo bila kuvaa barakoa au kuweka umbali kati yenu. Lakini kama uko pamoja na watu ambao hawajapata chanjo, bado unahitaji kuvaa barakoa, kukaa umbali wa futi sita kutoka kwao, na kunawa mikono mara nyingi.

Greater Lowell Health Alliance: greaterlowellhealthalliance.org/covid-19

Lowell Community Health Center: lhealth.org/patients/covid-19-updates

CDC: cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/vaccines/faq.html

MA DPH: mass.gov/info-details/covid-19-updates-and-information#covid-19-vaccine-

Mpango huu unategemeza na fedha kutoka kwa Hazina ya Greater Lowell Community Foundation ya Kukabiliana na Dharura ya COVID-19



GLHA
GREATER LOWELL HEALTH ALLIANCE



#ThisIsMyWhy

*Fonte: CDC | Rev. 3/10/21